



OFISI YA RAIS - TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA MOROGORO
SHULE YA SEKONDARI KIBUNGO JUU S.L.P. 802, SIMU: 0757201281 / 0703505557
TAREHE: _____

Jina la mwanafunzi _____

S.L.P. 802,
MOROGORO.

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIBUNGO JUU HALMASHAURI
YA WILAYA YA MOROGORO MKOA WA MOROGORO MWAKA 2021**

- 1.0 Utangulizi:**
Ninayofuraha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari ya Kibungo juu kwa mwaka 2021. Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 11/01/2021 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 19/01/2021. Mwanafunzi asiporipoti ndani ya siku zilizopangwa bila taarifa mzazi au mlezi wake atachukuliwa hatua kali za kisheria.
- 2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia**
- 2.1 Sare za Shule**
(a) Sare ya shule hii ni Shati jeupe mikono mifupi na suruali rangi ya bluu nyeusi (dark blue) kwa wavulana na wasichana shati jeupe mikono mifupi na sketi rangi ya bluu nyeusi (dark blue).
Nb: wazazi simamieni ushonaji wa sketi na suruali za vijana wenu, hatuta pokea mwanafunzi atakaekuja na sare isiyokubalika.
- 2.2 Maelezo ya mshono**
(a) Wasichana. Sketi ndefu inayovuka magoti kwa kiwango kikubwa (kutoka kwenye kifundo cha mguu chini isizidi sm5) na shati jeupe mikono mifupi. Kwa wanaoava Hijabu rangi ya Hijabu ni nyeupe.
(b) Wavulana. Suruali ndufu zenye rinda (Tahadhali isiwe modo haita kubaliwa) na shati jeupe mikono mifupi.
(c) T-shirt na sweta zitapatikana shuleni.
(d) Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba kwa wote.
(e) Soksi nyeupe kwa wote.
- 2.3 Mahitaji ya kitaaluma**
Mwanafunzi anatakiwa kuwa na daftari zisizo pungua 9, (Counter book) au daftari zozote kubwa kwa matumizi ya sekondari, na daftari za mazoezi na mitihani zisizo pungua 10, kalamu za kutosha, Mkebe wa hesabu pamoja na rula.
Nb: Kila mwanafunzi siku ya kuripoti ni lazima aje na peni zisizopungua mbili peseli moja na rula moja vifaa hivyo vitakaguliwa ili kuepusha tabia ya kuibiana..

2.3 Mahitaji mengine

- Mkanda mweusi kwa wavulana.
- Suruali yeusi kwa wavulana na sketi yeusi kwa wasichana kwa ajili ya shughuli za shamba.
- Track suite nyeusi au bukta na fulana za rangi ya bluu (jezi ya timu ya taifa ya bluu) kwa ajili ya michezo.

NB: Tunashauri kila mwanafunzi awe na sare za shule mbili ili kuepuka kuchakaa mapema.

3.0. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

3.1. Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na-25 ya mwaka 1978 na kama ilivyolekebishwa sheria ya Elimu Na 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote iliyotolewa na Wizara ya Elimu yenye dhamana na Elimu nchini na ofisi ya TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-

- (a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla jambo la lazima.
- (b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
- (c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- (d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- (e) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
- (f) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
- (g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- (h) Kutunza na kulinda mali za shule ni jukumu la kila mwanafunzi.


3.2. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha ufukuzwe shule.

1. Wizi.
2. Uasherati, ubakaji, Ushoga.
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.
4. Uvutaji bangi.
5. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi.
6. Kupigana na kupiga.
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma.
8. Kudharau Bendera ya Taifa.
9. Kuoa au kuolewa.
10. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
11. Kutoa mimba.
12. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
13. Kukataa adhabu kwa makusudi.

4.0. Mambo mengine muhimu.

Endapo mwanafunzi anatatizo lolote la kiafya mzazi au mlezi atoe maelezo kwa maandishi taarifa hiyo ipitishwe na mwalimu mkuu katika shule aliyotoka mwanafunzi.

"KARIBU SANA KIBUNGO JUU SEKONDARI"



MKUU WA SHULE
KABWEMA, F. J

THE HEADMASTER
KIBUNGO JUU SECONDARY SCHOOL
P. O. Box 802
MOROGORO